1977>>Mwaka ambao Chama

MZALENDO

# Madereva walioadhibiwa wawe mfano kwa wote wasiotii sheria nchini

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limetangaza kufungia leseni za udereva 42 kutokana na kubainika kukiuka sheria na kusababisha ajali.

Madereva hao wamefungiwa leseni katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, mkoani Mbeya, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Notker Kilewa, madereva hao walifungiwa leseni kufuatia 'kuchezea' mfumo wa VTS, unaowekwa katika mabasi ya abiria na Mamlaka ya Usafiri Ardhini (LATRA), kufuatilia mwendo wa vyombo vya usafiri.

Katika idadi hiyo ya madereva walioadhibiwa, 26 wamefungiwa leseni baada ya kubainika wamefanya makosa hayo katika mfumo wa VTS na wengine ulevi.

Tunalipongeza Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa uamuzi huo hapana shaka utasaidia kuwafanya madereva wote nchini, kuendesha magari kwa kufuata sheria za usalama barabarani.

Pia, tunawashauri madereva waliofungiwa leseni hizo, kwao iwe funzo kuhakikisha wakati mwingine hawafanyi makosa yanayogharimu uhai wa watu na mali zao.

Hivyo, tunawashauri wakati huu ambao wamefungiwa leseni waendelee kusoma sheria za usalama barabarani, kujikumbusha walipokosea pindi wakifunguliwa wasirudie makosa waliyofanya awali.

Aidha, adhabu hiyo ya polisi dhidi ya madereva wakorofi iwe salamu dhidi ya madereva wote wanaoendesha vyombo vya moto bila kuzingatia sheria, wafahamu serikali ipo macho wakati wote kumkamata na kumwadhibu dereva yeyote anayetenda makosa ya kizembe.

Tunaunga mkono kauli ya Naibu Kamishna wa Polisi, Fraisser Kashai kutoka Kamisheni ya Operesheni na Mafunzo aliyefanya ukaguzi wa mabasi ya abiria kabla ya kuanza safari katika stendi kuu ya jiji la Mbeya, juzi, kwamba madereva wanatakiwa kuheshimu na kutii sheria za usalama barabarani kwa lengo la kuepuka ajali.

Tunasisitiza dereva asiyetaka kuheshimu sheria tafsiri yake hayupo tayari kuepuka ajali zinazosababisha vifo vya watu wengi na kuziacha familia zikiwa yatima baada ya kupoteza baba, mama, watoto, ndugu, jamaa au marafiki ajalini huku wengine wakibaki na vilema vya kudumu.

Rai yetu, madereva wazuri wawe mabalozi wa kwanza kuwaelimisha wenzao kuhusu umuhimu wa kuheshimu sheria za usalama barabarani na yeyote atakayebainika anakaidi matakwa ya sheria, wasisite kumripoti katika vyombo vya dola kuhakikisha anashughulikiwa kwa mujibu wa sheria kuzuia ajali.

CamScanner

# Wadau waombwa kuwapa elimu ya usalama madereva bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi Tanzania kupitia Kitengo cha Usalama Barabarani limeitaka jamii kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali katika kutoa elimu kwa waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda kuhusu usalama barabarani, kusaidia kupunguza ajali na kuokoa maisha.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Operesheni wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Joseph Mwakabonga jana Dar es Salaam kwa niaba ya Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Taifa, William Mkonda.

Mwakabonga alitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya kitaifa ijulikanayo kama 'Chuma kwa Chuma Sio Poa', iliyoandaliwa na Kampuni ya Oryx Energies Tanzania, yenye lengo la kuongeza uelewa na kukuza tabia salama kwa waendesha bodaboda kote nchini.

Alisema elimu kwa umma ni jukumu la pamoja na kuzitaka sekta zote kushiriki kikamilifu katika kuwaelimisha waendesha pikipiki kuhusu usalama barabarani.

"Elimu ni msingi muhimu wa kuwasaidia waendesha pikipiki kuachana na tabia ya kuvunja sheria za usalama barabarani, ambayo ndiyo chanzo kikuu cha ajali," alisema.

Aidha, aliishukuru Oryx Energies Tanzania kwa kuunga mkono jitihada hizo kwa kugawa vifaa vya usalama barabarani kama vile kofia ngumu, vizimia moto na vifaa vingine vya kujikinga ili kupunguza majeraha na vifo vitokanavyo na ajali.

Kupitia kampeni hiyo, Oryx Energies pia ilitoa vibanda vitano vya kisasa vinavyotumia nishati ya jua kwa ajili ya askari wa usalama barabarani, vikatakavyowalinda dhidi ya jua na mvua wakiwa kazini, na hivyo kuboresha mazingira yao ya kufanyia kazi barabarani.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Oryx Energies Tanzania, Imani Mtafya alisema kampeni hiyo inalenga kuongeza uelewa na kuleta mabadiliko chanya ya tabia miongoni mwa waendesha bodaboda, bajaji na watumiaji wengine wa barabara.

Alisema malengo ya kampeni hiyo ni kutoa elimu ya usalama barabarani kwa waendesha bodaboda na bajaji kwa kushirikiana na polisi, kusambaza vifaa vya usalama.

Alitaja vifaa hivyo kuwa ni vibanda vya jua, kofia ngumu, vizibao vya kionekano, vizimia moto na vilainishi bora, na kutoa mafunzo ya usalama kwa zaidi ya waendesha usafiri 200 katika kila wilaya za Dar es Salaam, na baadaye nchi nzima.

"Ajali nyingi zinaweza kuzuilika. Elimu na uwajibikaji ndizo silaha zetu kuu," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Oryx Gas Tanzania Limited (OGTL), Benoit Araman alisema kampeni hiyo inalenga kuwapa maarifa ya usalama barabarani zaidi ya waendesha bodaboda na bajaji 200 kila wilaya za Dar es Salaam kabla ya kuenea nchi nzima.

"Tunaamini kuwa kwa kushirikiana, tunaweza kupunguza ajali, kuokoa maisha, kuhamasisha nishati safi na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi yetu," alisema Araman.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Waendesha Bodaboda, Saidi Kagomba aliwashukuru polisi kwa juhudi zao za kutoa elimu ya usalama barabarani.

Alisisitiza kuwa ni muhimu elimu hiyo itolewe mara kwa mara kwani waendesha bodaboda wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu sheria na kanuni za usalama barabarani.

CamScanner

PG 4



# Waendesha pikipiki watakiwa kujifunza sheria za usalama

Na Ally Ruambo

WAENDESHA pikipiki zikiwemo za matairi matatu 'bajaji' nchini wametakiwa kujifunza sheria za usalama barabarani na maarifa ya kutumia barabara wakati wakitekeleza majukumu yao ya usafirishaji.

Mkuu wa Usalama Barabarani Chang'ombe, Reverent Nkyami alitoa mwito huo jana wilayani Temeke wakati wa uzinduzi wa kilainishi kipya kwa ajili ya pikipiki na bajaji cha Caltex Ezy 4T Plus.

Nkyami alisema ukosefu wa mafunzo rasmi na elimu ya usalama barabarani imesababisha waendashaji wengi wa pikipiki kuendesha vyombo hivyo bila kujali sheria hali inayosababisha majanga na ajali za barabarani.

"Madereva wasiingie barabarani kama hawana maarifa ya kutumia barabara, kinachotokea sasa hivi mtu anajifunza siku mbili mtaani kesho anaingia barabarani na mbaya zaidi anapakia mishikaki (zaidi ya mtu mmoja) na kwa sababu hana weledi wa kutumia barabara anatembea hovyo anagongwa na kusababisha vifo," alisema.

Alisema Jeshi la Polisi limeendelea na utoaji elimu pamoja na operesheni mbalimbali ili kuongeza uelewa kwa madereva na kupunguza ajali za barabarani.

"Elimu tunazotoa zimesaidia kupunguza ajali za barabarani na ndiyo maana tunajikita sana kutoa elimu kwa waendesha pikipiki kwa sababu ajali nyingi zinahusisha pikipiki na waenda kwa miguu, pikipiki na magari, pikipiki kwa pikipiki na pikipiki kwa bajaji," alisema.

Aidha, Nkyami aliwataka waendesha pikipiki kushiriki mafunzo yanayoendeshwa na Jeshi hilo ili kuongeza uelewa na kujikinga na ajali za barabarani.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkuu wa Kitengo cha Vilainishi Kampuni ya Karimjee Value Chain Limited, Anam Mwemutsi alisema kampuni hiyo imeamua kuja na bidhaa hiyo kutokana na uchakachuaji mkubwa unaofanyika katika soko la vilainishi.

Mwemutsi alisema bidhaa hiyo ni rafiki kwa mazingira na pia itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji, ikiwemo kubadilisha vilainishi kila wiki kwa sababu bidhaa hiyo inaweza kutumika hadi mwezi mmoja.

"Utafiti tuliofanya mara nyingi bodaboda anasafiri kati ya Kilometa 900 hadi 1,200 kwa wiki sisi tumeleta kilainisha ambacho unaweza kwenda Kilometa 5,000 kwa hiyo unaweza kubadilisha mara moja tu kwa mwezi," alisema.

Naye Msemaji Msaidizi wa Shirikisho la Waendesha Bodaboda na Bajaji Mkoa wa Dar es Salaam, Saidi Msisiri alisema kilainishi hicho kitasaidia vyombo vyao kuwa salama na kuepukana na vilainishi ambavyo vimechakachuliwa.